



Mpangilio wa kupasha tohara ya kimatibabu kwa wanaume isiyo ya lazima

Hatua ya 1




Fika ili utahiriwe. Wewe pamoja na mshirika wako mnafaa kuelewa utaratibu, kwa hivyo ni vyema kwako na mshirika wako kumtembelea mshauri au muhudumu wa afya pamoja.

Hatua ya 2



Jadili kuhusu tohara ya kimatibabu kwa wanaume isiyo ya lazima na mshauri.

Hatua ya 3



Jaza fomu ya ombi la kupashwa tohara yakimatibabu kwa wanaume isiyo ya lazima.

Hatua ya 4



Pimwa viini vya UKIMWI

Hatua ya 5




Ukaguliwe kama una magonjwa yoyote kwenye viungo vya uzazi.

Hatua ya 6



Upewe sindano ya kutia ganzi sehemu ya chini ya uume wako kuifanya ife ganzi.

Hatua ya 7



Ngozi ya uume inatolewa.

Hatua ya 8




Upokee ushauri kuhusu unayopaswa kufanya ili upone vizuri.

Hatua ya 9




Pumzika kwa dakika 30.

Hatua ya 10



Nenda nyumbani. Usiendeshe baiskeli ukienda nyumbani, hata hivyo, kwa sababu inaweza kurarua kidonda na kuzuia kupona vizuri.

Hatua ya 11



Oga kwa uangalifu bila kulowesha bandeji.

Hatua ya 12



Toa bandeji baada ya siku 3 au tembelea kituo cha afya kilichoko karibu nawe kwa usaidizi kama huwezi kutoa bandeji mwenyewe.

Hatua ya 13



Usijichoshe na kazi au kuogelea kwa juma moja.

Hatua ya 14



Rudi katika kliniki siku ya 7 baada ya kutahiriwa ili ukaguliwe.

Hatua ya 15



Jiepushe na ngono au kupiga punyato kwa majuma sita ili upone vizuri



Republic of Kenya
Ministry of Public Health & Sanitation



USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE